# MTAALA WA SHULE YA JUMAPILI KWA AJILI YA WATOTO

***unaotokana na Injili ya Marko***






Miradi mingine ya shirika letu, Tawi la Uganda na Tanzania, ipo Dodoma, Musoma na Mpanda na ofisi yetu kuu iko Dar es Salaam. Miradi hii inashughulikia lugha zifuatazo: **Kialagwa, Kibende, Kiburunge, Kiikizu, Kiikoma, Kijita, Kikabwa, Kikwaya, Kimbugwe, Kingoreme, Kipimbwe, Kirangi, Kisandawe, Kisimbiti, Kitemi, Kizanaki, Kizinza.**

Huduma ya Kutafsiri Biblia na Kuendeleza Lugha za Asili, Mbeya

Ofisi ipo: Karibuni Centre, Maghorofani, Forest, Mbeya.

Namba ya simu: 025 250 0100



# MTAALA WA SHULE YA JUMAPILI KWA AJILI YA WATOTO

## *unaotokana na Injili ya Marko*

Huduma ya Kutafsiri Biblia
na Kuendeleza Lugha za Asili, Mbeya
S.L.P. 6359, Mbeya, Tanzania

Pamoja na

Wycliffe
*Partners in Bible Translation*

**Kichwa:** Mtaala wa Shule ya Jumapili kwa ajili ya watoto *unaotokana na Injili ya Marko* (Children's Sunday School Curriculum *based on Mark's Gospel*)

**Lugha:** Kiswahili

**Mwandishi:** Katherine O'Donnell

**Kimetafsiriwa na**: Katherine O'Donnell

**Mchoraji:** Gift Ngogo

**Mtaala umetengenezwa kwa msaada wa machapisho kutoka:** Claudia Smith

**'Utangulizi wa Injili kama ilivyoandikwa na Marko' umetengenzwa kwa msaada wa machapisho kutoka:** Andrew Pearson & Pioneer Bible Translators

**Maandiko yamechukuliwa kutoka:** Kiswahili Contemporary Version (Neno: Biblia Takatifu). © 2009 BIBLICA. Kwa Ruhusa ya BIBLICA. Haki zote zimehifadhiwa ulimwenguni kote.

Toleo la kwanza © 2018 Wycliffe Bible Translators, Inc.

## Kutumia lugha za asili

Tunapowafundisha watoto ni lazima tutumie lugha inayofaa – maneno rahisi, sentensi fupi na pia lugha inayotumika nyumbani. Kwa watoto wengine (hasa mjini) lugha inayotumika nyumbani ni Kiswahili, lakini kwa wengine (hasa kijijini) ni lugha ya asili. Lengo letu ni kwamba watoto wajifunze na kuelewa Neno la Mungu ili wamfahamu Mungu, kwa hiyo lazima tutumie lugha inayoeleweka na kutumika na watoto.

Siku moja tutasimama mbele ya Mungu na kumsifu kwa lugha zetu – kwa kweli kutumia lugha zetu (za asili na za taifa) zinaleta utukufu kwa Mungu wetu mbunifu, aliyeumba lugha hizi zote na kuziongea na kuzielewa zote!

> Baada ya haya nikatazama na hapo mbele yangu palikuwa na umati mkubwa wa watu ambao hakuna yeyote awezaye kuuhesabu. Kutoka kila taifa, kila kabila, kila jamaa na kila lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi na mbele ya Mwana-Kondoo.
>
> *Ufunuo 7:9*

"*Huduma ya Kutafsiri Biblia na Kuendeleza Lugha za Asili, Mbeya*" ipo kuwasaidia ninyi kutumia lugha za asili katika kuongea na Mungu na kumsikiliza, na pia katika kuwafundisha watoto. Vitabu vya Biblia, vitabu vingine na Maandiko yaliyorekodiwa vinapatikana kwa lugha zifuatazo: **Kibena, Kikinga, Kimalila, Kindali, Kinyakyusa, Kinyiha, Kisafwa, Kisangu na Kivwanji**. Tuko katika mchakato wa kuandaa vifaa kwa lugha za **Kibungu, Kikisi, Kimanda** na **Kipangwa**. Pia, huduma hii ipo kuwasaidia kujifunza kusoma lugha hizi na kuzitumia katika makanisa yenu na pamoja na watoto wenu.

Picha inayofuata inaonyesha mifano ya vitabu na vifaa vinavyopatikana. Vitabu vingi vingine vinapatikana katika ofisi zetu. Kuna vitabu vya Biblia (hasa vya Agano Jipya) pamoja na vitabu vidogo vya masimulizi ya Biblia vyenye picha na lugha rahisi. Tena kuna CD za Neno la Mungu. Pamoja na haya, kuna walimu wanaoweza kufundisha kusoma na kuandika lugha hizi za asili. Pia kuna walimu wanaoweza kufundisha walimu wa Shule ya Jumapili kwa ajili ya watoto na kutoa mafundisho mengine yanayohusu matumizi ya Biblia.

- Tukimfuata Mungu kwa namna hii, hatutakuwa na sababu ya kumwogopa Mungu. Atakuwa Baba yetu, na sisi tutakuwa watoto wake. Anaahidi kuwa hatatuacha kamwe, bali atatupenda daima.



# Mtaala wa Shule ya Jumapili kwa ajili ya watoto – *Unaotokana na Injili ya Marko*

## Utangulizi

Ni faida kubwa na pia jukumu kubwa kuwafundisha watoto ili wamfahamu Mungu. Tuwafundishe kwa makini tukiwasaidia kuelewa Neno la Mungu na kuona jinsi linavyogusa maisha yao. Tuwe mifano mizuri mbele ya watoto, ili waone kwa vitendo maana ya kumpenda na kumfuata Yesu.

Lengo la kitabu hiki siyo kukufanya uwe mwalimu mzuri, licha ya kwamba kuna mawazo yanayohusu kuwafundisha watoto vizuri. Bali, lengo la kitabu hiki ni kukupa mfululizo wa masomo yanayofaa kwa watoto na ambayo yanatokana na Injili ya Marko. Mtaala huu ni rahisi kuufuata, ili mwalimu yeyote aweze kuutumia.

## Kutumia mtaala

Mtaala huu unatokana na Injili ya Marko. Hata kama unacho kitabu cha Injili ya Marko tu kati ya vitabu vyote vya Biblia, bado utaweza kuwafundisha watoto kuhusu Yesu Kristo kwa kutumia mtaala huu.

### Masomo yanagawanyika kufuatana na dhamira zifuatazo:

- Mwanzo wa huduma ya Yesu (Masomo 1-5)
- Yesu ana uwezo juu ya vyote (Masomo 6-12)
- Mafundisho ya Yesu (Masomo 13-18)
- Kuwa ndani ya familia ya Yesu (Masomo 19-23)
- Kifo na ufufuo wa Yesu (Masomo 24-32)**

***Unaweza kuchagua kutumia masomo haya wakati wa Pasaka, hata kama ungepaswa kuruka masomo mengine. Baadaye utaweza kurudi kwenye masomo uliyoruka.*

### Kwa kila somo, mtaala huu unatoa:

- Kifungu cha Biblia cha kusoma
- Kweli kuu za kufundisha (vipengele vikuu vya simulizi)
- Jinsi somo linavyoweza kutumika katika maisha ya watoto
- Mstari wa kukumbuka

### Mambo ya kuzingatia katika kupanga somo:

- **Kuandaa somo kwa makini na fanya maombi:** Unapoandaa somo, ni muhimu kumwomba Roho Mtakatifu akufundishe wewe pamoja na kuwafundisha watoto. Kwa kuandaa somo mapema, utakuwa na muda wa kutosha kusoma kifungu cha Biblia kwa kina na kuomba. Pia kuwahi kuandaa kutakupa muda wa kuhakikisha unajua kila utakachofundisha, pamoja na kuandaa vitendea kazi vitakavyohitajika.
- **Kutumia Neno la Mungu kwa usahihi:** Kabla ya kuwafundisha watoto kifungu fulani cha Biblia, ni muhimu sana kusoma kifungu hicho wewe mwenyewe, ili kuhakikisha umekielewa vizuri. Baada ya kukitafakari kifungu, unatakiwa kufikiri jinsi utakavyokifundisha kwa namna itakayoeleweka kwa watoto na kugusa maisha yao. Vipengele vya ‘Kweli kuu za kufundisha’ na ‘Jinsi somo linavyoweza kutumika’ vitakusaidia katika kufanya hivyo.
- **Kuwashirikisha watoto:** Kuwashirkisha watoto kutawasaidia watoto kusikiliza na kujifunza. Watoto wawe na nafasi za kuongea, kuona na kufanya, pamoja na kusikiliza. Uwe na shughuli mbalimbali kwenye somo zitakazoimarisha somo unayofundisha.
- **Umri wa watoto:** Kama watoto ni wadogo, wataweza kusikiliza kwa muda mfupi tu na hivyo wawe na muda mwingi wa kucheza. Lakini kama watoto ni wakubwa wataweza kutulia na kusikiliza kwa muda mrefu zaidi. Pia watoto wakubwa wapewe nafasi ya kutafakari kwa kina kwa kuuliza na kujibu maswali, na wengine wataweza kusoma kifungu cha Biblia wao wenyewe.
- **Kutumia lugha inayoeleweka:** Utumie maneno rahisi na lugha nyepesi na kuhakikisha watoto wanakusikia vizuri. Pia utumie lugha ambayo watoto wanatumia nyumbani (ambayo inaweza kuwa lugha ya asili badala ya Kiswahili).

Hapo chini utaona mwongozo unaoweza kutumia katika kuandaa somo ambalo litakuwa la kuvutia na la Biblia, ukitumika pamoja na mtaala huu.

## Mwongozo kwa ajili ya somo la Shule ya Jumapili

Hiyo ndiyo njia moja ya kuunda somo lako:

1. **Shughuli ya mwanzo:** Kwa mfano, cheza mchezo, imba nyimbo au chora picha (zinazohusiana na somo) na kupaka rangi.



## Kuwaelezea watoto maana ya kuwa Mkristo

Kuwasaidia watoto kuelewa maana ya kuwa Mkristo, utahitaji kuwaelezea yafuatayo:

- Mungu ni Mtakatifu – hakuna wa kufanana naye.
- Mungu ni Muumbaji – alituumba kwa mfano wake.
- Mungu anawapenda wote aliowaumba, anatamani awe na uhusiano wa karibu nao.
- Mungu ametupatia kazi ya kutunza vitu vyote alivyoumba duniani.
- Lakini watu hupenda kufanya kama wanavyotaka, badala ya kufuata mapenzi ya Mungu; wanamkosea Mungu, hawamheshimu Mungu. Kufanya hivi kunaitwa ‘dhambi’.
- Adamu na Hawa walikuwa wa kwanza kutenda dhambi, na sisi sote tunatenda dhambi pia.
- Kwa kuwa Mungu ni Mtakatifu, huchukia dhambi. Kwa hiyo, dhambi huvunja uhusiano kati yetu na Mungu. Matokeo ya mwisho ya dhambi ni kifo.
- Kwa kuwa Mungu ni Pendo, hutaka kurudisha uhusiano kati yetu. Anataka kuwa Baba yetu na kuwa pamoja nasi milele na milele.
- Kwa hiyo, Mungu alimtuma Mwana wake wa pekee, Yesu, aishi kama binadamu na kufa msalabani. Alichukua nafasi yetu msalabani, akafa kwa ajili yetu kwa kubeba dhambi zetu na kuadhibiwa kwa niaba yetu.
- Tukiamini haya yote kuwa kweli na kumpenda Mungu na kutaka kuwa na uhusiano wa karibu naye, Mungu yuko tayari kutusamehe. Biblia inasema kwamba atasahau dhambi zetu, kwa sababu Yesu alizibeba msalabani. Hii inaitwa ‘wokovu’.
- Kuokolewa si matokeo ya juhudi zetu, bali ni kwa neema ya Mungu, kupitia kifo cha Yesu msalabani, kutokana na upendo wake mkuu (Yohana 3:16).
- Tukiokolewa, hatutakufa kiroho (hata kama siku moja tutakufa kimwili). Mungu ataishi ndani yetu kwa njia ya Roho wake Mtakatifu na hatimaye tutakuwa pamoja na Mungu.
- Tukimpenda Mungu na kumheshimu, itabadilisha maisha yetu yote – tutataka kumpendeza Mungu siku zote, katika kila tunachofanya. Tutataka kumsikiliza (kwa kusoma au kusikiliza Biblia) na kuongea naye (kwa kuomba na kuimba) kila siku.

## 31. Yesu anawatuma wanafunzi wake na kupaa mbinguni – Marko 16:14-20

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu aliwapa wanafunzi wake kazi ya kuenda ulimwenguni kote na kuwatangazia watu habari zake: Wawatangazie wote kuhusu upendo wa Mungu, habari njema ya msalaba na jinsi ya kuishi maisha ya kumfuata Yesu (yaani, kuwa Wakristo).

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Sisi pia, tukiwa Wakristo, tumepewa kazi muhimu ya kuwatangazia wengine habari za Yesu. Je, wewe utaweza kumwambia nani kuhusu Yesu wiki hii?
- Waombee wamishenari, wahubiri, wainjilisti na wengine wanaowatangazia watu habari za Yesu.

***Mstari wa kukumbuka:*** Akawaambia, "Nendeni ulimwenguni kote, mkawahubirie watu wote Habari Njema." (Marko 16:15)

## 32. Somo la marudio

Kabla hujaanza kufundisha kitabu kingine cha Biblia, urudie masomo yote yanayohusu 'Kifo na ufufuo wa Yesu'. Unaweza kuchagua kufanya hivi kupitia chemsha bongo: Uwagawanye watoto katika timu mbili na kuwauliza maswali yanayohusu mambo yote waliyojifunza. Uanze na maswali yanayohusu somo la kwanza, na kuendelea kwa kuuliza maswali katika mpangalio wenye mantiki. Timu inayofanikiwa kujibu maswali mengi kwa usahihi kuliko timu nyingine imeshinda. Pia warudie mistari yote ya kukumbuka. Uwahamasishe watoto wakubwa wasome kitabu kizima cha Marko nyumbani.

## Kuwasilisha waliyojifunza

Kwa kuwa mmefika mwisho wa kitabu cha Marko, ni wakati mzuri wa kuomba viongozi wa kanisa wawapatie watoto nafasi ibadani ya kuliambia kanisa kuhusu waliyojifunza. Uwasaidie watoto kujiandaa kuwasilisha waliyojifunza kutoka katika kitabu cha Marko kuhusu Yesu na jinsi ya kumfuata. Pia uchague mistari kadhaa kati ya mistari ya kukumbuka waliyojifunza, ili watoto waikariri ibadani.



2. **Rudia walichojifunza wiki zilizopita:** Kabla hujaanza kufundisha jambo jipya, uhakikishe watoto wamekumbuka somo la wiki iliyopita na hata wiki zingine zilizopita, kwa kuwauliza maswali. Ni muhimu sana kufanya hivi, kwa sababu mtaala huu unafuata mfululizo wa masomo, na kila somo linategemea masomo yaliyopita (yaani, kila somo linajenga juu ya somo lililopita). Hivyo, ni lazima kuwasaidia watoto kukumbuka mahali mlipofikia katika kusoma kuhusu maisha ya Yesu, na kuhusianisha somo lililopita na somo linalofuata.
3. **Utangulizi:** Tafuta njia ya kutambulisha habari za Biblia mtakazosoma ili watoto wavutiwe na kutamani kuzisikiliza.
4. **Maombi:** Omba Mungu awasaidie watoto kuelewa Neno lake.
5. **Simulia habari ya Biblia:** Tumia kifungu cha Biblia kilichotolewa kwenye mtaala. Simulia habari kutoka katika kifungu hicho kwa namna itakayovuta usikivu wa watoto, kwa kutumia vitendo, kuwashirikisha watoto na kuwauliza maswali. Mara nyingi ni bora kusimulia habari kwa maneno yako mwenyewe, badala ya kusoma moja kwa moja kutoka kwenye Biblia, ili uweze kusimulia kwa lugha nyepesi na kwa kifupi. Lakini, kama unawafundisha watoto wakubwa ni vizuri kuwashirikisha kwa kuomba wasome kifungu husika cha Biblia.
6. **Mafundisho/Maelezo ya simulizi:** Mara baada ya kusimulia habari ya Biblia, utahitaji kuwasaidia watoto kuelewa maana yake na jinsi inavyogusa maisha yao. Ili kufanya hivyo, utumie 'Kweli kuu za kufundisha' na 'Jinsi somo linavyoweza kutumika' zinazotolewa katika mtaala huu. Unapofundisha uwashirikishe watoto kwa kuwauliza maswali, kwa kutumia vielelezo na kwa kutoa mifano kutoka katika maisha yao ya kila siku.
7. **Mstari wa kukumbuka:** Tumia 'Mstari wa kukumbuka' unaotolewa katika mtaala huu (watoto wajifunze mstari huu kwa lugha wanayotumia nyumbani, yaani lugha yao ya asili). Wakati mwingine utaona mstari fulani unarudiwa – kurudia mstari kwa namna hii kunawasaidia watoto kuushika vizuri. Kama watoto wamesahau mstari wa wiki iliyopita, ni bora kuurudia kuliko kujifunza mstari mpya. Mistari yote ya kukumbuka inatoka katika kitabu cha Marko. Lakini, wakati mwingine utaona kuna mstari mwingine unaotajwa kutoka katika kitabu kingine cha Biblia ambao unaweza kutumia kama vitabu hivi vinapatikana katika lugha yako (watoto wasijifunze mistari yote miwili, bali uchague mstari mmoja kati hiyo). Uwasaidie watoto kushika mstari kwa kutumia vitendo au kwa kuimba.

8. **Marudio:** Hakikisha watoto wameelewa somo na wataweza kulikumbuka vizuri kwa kufanya shughuli ya kurudia somo. Shughuli hiyo ya marudio inaweza kuwa chemsha bongo, mashindano, kuchora na kupaka rangi, kutengeneza kitu (sanaa), igizo au hata mchezo.
9. **Maombi:** Omba Mungu amsaidie kila mmoja kukumbuka na kutumia kila alichojifunza. Kama watoto ni wakubwa, unaweza kuchagua kuwashirikisha katika kuomba kwa kuwapa nafasi ya kutaja maombi yao na kuyaombea wenyewe.
10. **Shughuli za mwisho:** Kama kuna muda unaobaki, unaweza kuutumia kucheza michezo au kuimba nyimbo zinazohusiana na somo. Ni vizuri kumaliza somo kwa kurudia mstari wa kukumbuka kwa mara ya mwisho.

## Utangulizi wa Injili kama ilivyoandikwa na Marko

Injili kama ilivyoandikwa na Marko ni kitabu kimojawapo kati ya vitabu vinne vya kwanza katika Agano Jipya vinavyoelezea maisha ya Yesu Kristo. Kila kimoja, katika vitabu hivyo vinne, kinaitwa 'injili'. Maana ya neno injili ni 'habari njema'. Vitabu hivi viliandikwa baada ya Yesu kurudi mbinguni.

Waandishi wa vitabu hivyo walikuwa ni Mathayo, Marko, Luka, na Yohana. Injili kama ilivyoandikwa na Marko ndiyo kitabu kifupi zaidi miongoni mwa injili hizo nne. Pia inaaminika kuwa katika injili hizo nne, injili ya Marko ndiyo ilitangulia kuandikwa.

Huyu Marko, ambaye pia anajulikana kama Yohana Marko, alikuwa mfuasi wa Mtume Paulo na Barnaba. Baadaye Marko alikuwa rafiki mkubwa wa Petro (1 Petro 5:13).

Katika kitabu hiki anaeleza mengi ambayo alikuwa anafanya Yesu kuzidi ambayo alikuwa anahubiri. Tunaiona miujiza mingine ambayo alifanya Yesu, aliponya watu, alitoa pepo wachafu na kuwasamehe watu dhambi. Hayo yanaonyesha mamlaka ya Yesu, kuwa alitoka kwa Mungu, kuja kutoa uzima wake kuwafungua watu kutoka katika nguvu ya dhambi.

***Muhtasari wa kitabu***

1. Utangulizi wa kitabu, 1:1-13.
2. Huduma ya Yesu Galilaya, 1:14-8:21.
3. Safari ya Yesu kuelekea Yerusalemu, 8:22-10:52.
4. Huduma ya Yesu Yerusalemu, kifo na kufufuka kwake, 11:1-16:8.



***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Alipokufa msalabani, Yesu alibeba adhabu ya kifo kwa ajili ya dhambi zetu. Kwa kuwa Yesu alikufa hivyo, sisi hatupaswi tena kupokea adhabu hiyo. Tunapoomba msamaha na kumkubali Yesu kuwa Mwokozi wetu, dhambi zetu hufutwa kabisa. Tunaweza kuanza maisha mapya na Yesu.
- Mshukuruni Mungu kwa Yesu, kwa jinsi alivyobeba dhambi zetu msalabani.
- Kama mtoto yeyote ameelewa vizuri maana ya kifo cha Yesu na kutaka kumfuata Yesu, apewe nafasi ya kuomba na kukabidhi maisha yake kwa Mungu.
- ***Mwalimu:*** *Tumia muda wa kutosha kuhakikisha watoto wameelewa kwa kina maana ya kifo cha Yesu na maana ya kuwa Mkristo. (Mwishoni pa mtaala huu utakuta mwongozo wa kukusaidia kuwaelezea watoto maana ya kuwa Mkristo). Unaweza kuchagua kutumia zaidi ya wiki moja kufundisha somo hili, ili kuhakikisha watoto wameelewa kwa kina.*

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 10:45 & Marko 2:10 *(Au Yohana 3:16 Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu kiasi cha kumtoa Mwanae pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.)*

## 30. Kufufuka kwa Yesu – Marko 16:1-14

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu yu hai!
- Kufufuka kwa Yesu kunathibitisha kuwa Yesu ni Mungu. Yesu ana nguvu juu ya kifo.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Sisi tunaweza kuwa na maisha mapya na Yesu kwa sababu Yesu alifufuka na yu hai. Hata kama tutakufa, kifo si mwisho. Kwa Wakristo, kifo ni mwanzo wa uhai wa milele na kuwa pamoja na Baba yetu mbinguni anayetupenda sana.
- Msifuni Mungu na kusherehekea kuwa Yesu yu hai. Yesu ameshinda dhambi na mauti, kwa hiyo sisi hatuna sababu ya kuogopa kifo.

***Mstari wa kukumbuka:*** "Msishtuke. Mnamtafuta Yesu Mnazareti, aliyesulubiwa. Amefufuka!"(Marko 16:6a) *(Au rudia Yohana 3:16)*

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Tunaposhirikiana katika Meza ya Bwana, mkate tunaokula na divai tunayokunywa zinatukumbusha juu ya kifo cha Yesu. Kufanya hivi kunatusaidia kukumbuka jinsi Yesu alivyotupenda sana hata kufa msalabani, ili sisi tuweze kuwa na urafiki na Mungu.
- Tumia muda kwa pamoja wa kumshukuru Yesu kwa upendo wake na kuomba msamaha kwa yale tuliyofanya yaliyomsikitisha Mungu na yaliyowaumiza wengine. Omba msamaha na kupokea zawadi ya uhai kupitia Yesu Kristo.

***Mstari wa kukumbuka:*** "Kwa maana hata mimi Mwana wa Adamu sikuja ili nitumikiwe, bali nilikuja ili niwe mtumishi na kutoa maisha yangu yawe fidia kwa ajili ya watu wengi." (Marko 10:45)

## 28. Kukamatwa kwa Yesu – Marko 14:43-46, 53-54, 66-72

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu alikamatwa. Alisalitiwa na mmoja wa wanafunzi wake, Yuda. Mwanafunzi mwingine, Petro, ambaye alikuwa rafiki wa karibu wa Yesu, alimkana Yesu.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Yesu anafahamu maumivu ya kuwa na rafiki mzuri anayesema, "Mimi siyo rafiki yako". Bila shaka, maneno na matendo ya Yuda na ya Petro yalimwumiza sana Yesu.
- Hivyo, ukiumizwa na maneno au matendo ya rafiki fulani, Yesu anaelewa maumivu yako. Unaweza kuchagua kuongea na Yesu kuhusu hali hiyo.
- Je, wewe ni rafiki wa namna gani? Je, utakuwa rafiki mwaminifu au utamkimbia rafiki yako akiwa na shida na kuhitaji msaada?

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 12:30-31

## 29. Kifo cha Yesu – Marko 15:22-47

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu aliteseka sana kwa ajili yetu. Kufa msalabani ni kifo cha maumivu makali sana. Tena alisikia maumivu makali sana kutokana na kubeba dhambi zetu zote na alifikiri kuwa Mungu, Baba yake, amemwacha.



# MTAALA

## Mwanzo wa huduma ya Yesu

## 1. Yohana Mbatizaji anaandaa njia – Marko 1:1-8

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yohana Mbatizaji alikuwa akiwaandaa watu kukutana na mtu maalumu sana, Yesu.
- Aliwaita watu watubu na kubatizwa kwenye maji kama ishara ya kuwa wanajitayarisha kukutana na Yesu. Kufanya hivi kulimaanisha kuwa walijutia yale waliyofanya ambayo yalimsikitisha Mungu na kutaka kubadilika.
- Yesu ni Mwana wa Mungu.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Je, uko tayari kukutana na Yesu? Katika wiki zijazo tutajifunza mambo mengi kuhusu Yesu.

***Mstari wa kukumbuka:*** Na sauti kutoka mbinguni ikasema, "Wewe ni mwanangu mpendwa; nimependezwa nawe." (Marko 1:11)

## 2. Kubatizwa kwa Yesu – Marko 1:9-13

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu alikulia katika kijiji cha Nazareti. Alipokuwa na miaka kama thelathini, alibatizwa.
- Yesu ni Mwana wa Mungu, Mpendwa wake, na Roho ya Mungu ilikuwa pamoja naye na kumsaidia kufanya yote ambayo Mungu alimtaka afanye.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Mwombe Mungu akusaidie, kupitia Roho Mtakatifu, kuishi kwa namna inavyompendeza.

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 1:11

## 3. Yesu anawachagua wanafunzi wake kumi na wawili – Marko 1:14-20; 3:13-19

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu aliwatangazia watu Habari Njema ya Mungu na kuwaita watubu na kuamini ahadi za Mungu.
- Yesu aliwaita watu kumi na wawili kuwa wanafunzi wake na marafiki zake wa karibu, ili wamsaidie katika kutangaza Habari Njema ya Mungu.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Je, unataka kumfuata Yesu na kuwatangazia wengine kuhusu Yesu? Unaweza kumwambia nani Habari Njema ya Mungu?

***Mstari wa kukumbuka:*** Yesu akawaambia, "Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu." (Marko 1:17)

## 4. Yesu akamwita Lawi, aliyekuwa mtoza ushuru, amfuate – Marko 2:13-17

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu alikuja kwa ajili ya watu wanaojitambua kuwa wenye dhambi, siyo kwa wale wanaojiona kuwa wema!

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Yesu anatupenda, licha ya mabaya tunayofanya. Je, utachagua kumfuata?
- Kumfuata Yesu kunamaanisha kumsikiliza, kumpenda na kumtii katika maisha yetu ya kila siku.

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 1:17

## 5. Somo la marudio

Kabla ya kuanza dhamira inayofuata, urudie masomo yote yanayohusu 'Mwanzo wa huduma ya Yesu'. Unaweza kuchagua kufanya hivi kupitia chemsha bongo: Uwagawanye watoto katika timu mbili na kuwauliza maswali kuhusu mambo yote waliyojifunza. Uanze na maswali yanayohusu somo la kwanza, na kuendelea kwa kuuliza maswali katika mpangalio wenye mantiki. Timu inayofanikiwa kujibu maswali mengi kwa usahihi kuliko timu nyingine imeshinda. Pia warudie mistari yote ya kukumbuka.



- Hawakuweza kuelewa kila kilichotokea na maana yake, lakini walijua wamsikilize Yesu na kufanya kila alichowaambia.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Sisi tunaweza kumsikiliza Mungu kupitia Neno lake, yaani Biblia. Tunapomtii Mungu na kufanya kila anachotuambia, tunaonyesha kuwa tumemsikiliza kweli.
- Omba Mungu akusaidie kuelewa kila unachosoma na kusikia kwenye Biblia.

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 8:34b

## 26. Yesu anaingia Yerusalemu kwa shangwe – Marko 11:1-11

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu ni Mfalme – Mfalme wa mbingu na dunia. Anastahili sifa zetu.
- Yesu alikuwa Mfalme mnyenyekevu; hakuwa na dhahabu au mali nyingi.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Ni vyema kumsifu Yesu na maneno yetu, kwa kuimba na kucheza.
- Imba wimbo wa kumsifu Mungu kwa pamoja na kucheza ili kuonyesha jinsi mnavyompenda.

***Mstari wa kukumbuka:*** "Hosana! Mungu apewe sifa! Mungu ambariki yeye anayekuja kwa jina la Bwana!" (Marko 11:9b)

## 27. Karamu ya Bwana – Marko 14:12-26

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu aliwatuma wawili wa wanafunzi wake Yerusalemu ili wafanye maandalizi ya Pasaka. (Pasaka ilikuwa karamu maalumu ya kukumbuka jinsi Waisraeli walivyokombolewa Misri. Karamu hii iliwakumbusha jinsi Mungu alivyowaokoa Waisraeli alipokuwa akituma pigo la mwisho la kuwaua wazaliwa wa kwanza wa Wamisri.)
- Habari hizi zinatusaidia kuelewa ni kwa sababu gani tunasherehekea 'Meza ya Bwana' (Ushirika Mtakatifu/Komunyo) kanisani. Yesu alitaka wanafunzi wake wakumbuke kifo chake msalabani. Hivyo, Yesu alitwaa mkate na kuumega kama ishara ya jinsi mwili wake utakavyoumia msalabani, kisha akatwaa kikombe cha divai kama ishara ya jinsi damu yake itakavyomwagika msalabani.

*muwe sadaka hai, takatifu na inayompendeza Mungu, ambayo ndio ibada yenu ya kiroho.)*

## 23. Somo la marudio

Kabla ya kuanza dhamira inayofuata, urudie masomo yote yanayohusu 'Kuwa ndani ya familia ya Yesu'. Unaweza kuchagua kufanya hivi kwa kumfanya kila mtoto achore picha ya habari fulani mliyosoma (kila mtoto achague habari anayotaka kuchorea). Kisha, baada ya kuchora, kila mmoja awaonyeshe wenzake alichochora na kuwaelezea kila anachokumbuka kuhusu habari hiyo. Pia warudie mistari yote ya kukumbuka.

# Kifo na ufufuo wa Yesu

## 24. Yesu anazungumza juu ya kifo chake – Marko 8:27-38

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu ni Kristo, aliyetumwa na Mungu kuwaokoa watu wake, kama Mungu alivyoahidi. Alijua kuwa atauawa lakini pia atafufuka. Yeyote anayetaka kumfuata Yesu awe tayari kuvitoa vitu vyake vyote kwa ajili yake, kama naye Yesu alivyotoa maisha yake kwa ajili yetu.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Wakati mwingine ni vigumu kumfuata Mungu. Kwa mfano, wakati mwingine marafiki zako wanakushawishi kufanya kitu ambacho kitamsikitisha Mungu, na hivyo unapaswa kuchagua kati ya mapenzi ya marafiki zako na mapenzi ya Mungu. Ni kwa namna gani zingine ambazo kumfuata Mungu ni vigumu? Je, utachagua kumfuata licha ya magumu haya?

***Mstari wa kukumbuka:*** "Mtu ye yote akitaka kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, anifuate." (Marko 8:34b)

## 25. Yesu anageuka sura – Marko 9:2-10

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Mara Petro, Yakobo na Yohana walipoona jinsi Yesu alivyogeuka sura mbele yao, na kusikia sauti ya Mungu, walijua ya kuwa Yesu ndiye Mwana wa Mungu.



# Yesu ana uwezo juu ya vyote

Sehemu hii ina mistari ya kukumbuka iliyo mirefu. Hivyo unaweza kuchagua kujifunza maneno yenye **maandishi mazito** tu au kutumia mstari ufuatao kwa masomo yote: "Kwa wanadamu haiwezekani, lakini kwa Mungu si hivyo. Mambo yote yanawezekana kwa Mungu." (Marko 10:27b)

## 6. Yesu anamponya mtu aliyepooza – Marko 2:1-12

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu ana mamlaka na uwezo wa kusamehe dhambi (kwa sababu yeye ni Mungu) na uwezo wa kuponya.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Tunaweza kumjia Yesu na kumwambia makosa yetu, na tunaweza kumwamini kuwa atatusamehe.

***Mstari wa kukumbuka:*** "Lakini ili kuwahakikishia kwamba **mimi Mwana wa Adamu ninao uwezo hapa duniani wa kusamehe dhambi**," akamwambia yule aliyepooza, "Nakuambia, inuka, chukua kitanda chako uende nyumbani." (Marko 2:10-11)

## 7. Yesu anatuliza dhoruba – Marko 4:35-41

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu ana uwezo juu ya hali ya hewa (kwa sababu vitu vyote viliumbwa naye).

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Tunapoogopa, tunaweza kumwambia Yesu. Yesu yuko pamoja nasi; hakuna sababu ya kuogopa.

***Mstari wa kukumbuka:*** Lakini wao walikuwa wamejawa na hofu wakaulizana, **"Ni nani huyu ambaye hata upepo na mawimbi vinamtii?"** (Marko 4: 41)

## 8. Yesu anamponya mtu mwenye pepo – Marko 5:1-20

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu ana uwezo juu ya pepo (kwa kuwa yeye ni Mwana wa Mungu).

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Yesu ana nguvu zaidi kuliko pepo yeyote, kwa hiyo tusiogope. Mwombe Mungu akulinde.

***Mstari wa kukumbuka:*** Yesu akawaponya watu wengi waliokuwa na magonjwa ya kila aina. Akawatoa pepo wengi. (Marko 1:34a)

## 9. Msichana anarudishiwa uhai na mwanamke kuponywa – Marko 5:21-43

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu ana uwezo juu ya magonjwa (kwa sababu anajua jinsi tulivyoumbwa).

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Tunaweza kumwomba Yesu awasaidie wagonjwa. Kama ni mapenzi yake, atawaponya.
- Omba kwa pamoja kwa yeyote ambaye ni mgonjwa.

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 1:34a

## 10. Yesu anawalisha watu elfu tano – Marko 6:30-44

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu ana nguvu ya kutupa ridhiki zetu zote. Yesu ni mwenye huruma. Yesu anawajali watu na mahitaji yao.
- Yesu alijali mahitaji yao ya kiroho (akawafundisha) na ya kimwili (akawapa chakula).

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Yesu ni wa ajabu! Kwa pamoja msifuni Mungu na kumshukuru kwa huruma zake na kwa kila kitu anachotupatia.
- Mwombe Yesu akufundishe pia, ili ukue kiroho pamoja na kimwili!

***Mstari wa kukumbuka:*** "Kwa wanadamu haiwezekani, lakini kwa Mungu si hivyo. Mambo yote yanawezekana kwa Mungu." (Marko 10:27b)



## 21. Yesu anawabariki watoto wadogo – Marko 10:13-16

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu aliwakaribisha na kuwabariki watoto wadogo. Mungu anawapenda watoto na watoto ni wa muhimu katika familia ya Mungu.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Unaweza kumjia Mungu wakati wowote, yeye yupo muda wote na yuko tayari kukusikiliza.
- Mungu anapenda kusikia habari zako za kila siku zinazohusu familia, marafiki, shuleni, mawazo yako n.k. Unaweza kuongea na Mungu kuhusu mambo yote!

***Mstari wa kukumbuka:*** "Waacheni watoto wadogo waje kwangu wala msiwazuie, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wa watu kama hawa!" (Marko 10:14b)

## 22. Yesu anapakwa marashi (perfume) – Marko 14:1-9

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Mwanamke huyu anatupa mfano mzuri wa maana ya kumwabudu Mungu. Marashi hayo yalikuwa gharama kubwa, lakini mwanamke alimtia Yesu marashi hayo kichwani kwa furaha, kwa kuwa alimheshimu Yesu sana.
- Tunamwabudu Mungu na maisha yetu yote – siyo kwa maneno yetu tu bali pia kwa vitendo vyetu.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Tunapoenda kanisani, wakati mwingine inatugharimu – siyo kwa fedha bali kwa muda wetu na jitihada zetu, hasa tukichoka na kutamani kusinzia au tukitaka kubaki nyumbani ili kucheza. Lakini Mungu anafurahi tunapomjia na kumwabudu kwa maneno yetu na vitendo vyetu.
- Sasa, mmwabudu Mungu kwa pamoja – msifuni kwa kumwambia jinsi alivyo wa ajabu.
- Unaweza kumtendea Mungu nini ili kuonyesha jinsi unavyomheshimu na kumpenda?

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 12:30-31 *(Au Warumi 12:1 Kwa hiyo ndugu zangu nawasihi kwa sababu ya huruma zake Mungu, jitoeni kwake*

## Kuwa ndani ya familia ya Yesu

### 19. Yesu anaomba/anasali – Marko 1:35-37 na Marko 6:45-46

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu alitumia muda na Baba yake kwa kuomba.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Mungu ana furaha kubwa tunapomjia na kuongea naye. Tunaweza kuomba/kusali mahali popote na wakati wowote.
- Njia moja ya kuunda maombi yako kwa utaratibu ni kutumia 'S' hizi nne: Sifa, Shukrani, Samahani, Shida.
    - **S**ifa: Msifu Mungu kwa jinsi alivyo.
    - **S**hukrani: Mshukuru Mungu kwa yote aliyokutendea.
    - **S**amahani: Tubu dhambi zako na kuomba msamaha.
    - **S**hida: Kabidhi shida na haja zako na za wengine mikononi mwa Mungu na kuomba msaada wake.

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 1:11 *(Au Wafilipi 4:6 Msifadhaike juu ya jambo lolote; lakini katika kila jambo mjulisheni Mungu haja zenu, kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru.)*

### 20. Mama na ndugu za Yesu – Marko 3:31-35

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu alisema kuwa yeyote anayempenda Mungu na kumtii ni katika familia ya Mungu.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Familia ni za muhimu. Ni jambo jema kutumia muda na familia zetu. Kwa hiyo, ukimpenda na kumtii Mungu, ni vizuri kutumia muda naye na familia yake. Tunaweza kufanya hivi kwa njia gani?

***Mstari wa kukumbuka:*** "Mtu ye yote anayetenda mapenzi ya Mungu ndiye ndugu yangu na dada yangu na mama yangu." (Marko 3:35)



### 11. Kuponywa kwa kipofu Bartimayo – Marko 10:46-52

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu ana uwezo juu ya magonjwa. Anaweza kuwafanya vipofu waone (vipofu wa kimwili pamoja na vipofu wa kiroho).
- Mara alipoweza kuona, Bartimayo alianza kumfuata Yesu.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Mwombe Mungu atusaidie kuona (yaani, kuelewa) mambo ya kiroho, ili tuweze kumfuata Yesu.

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 10:27b

### 12. Somo la marudio

Kabla ya kuanza dhamira inayofuata, urudie masomo yote yanayohusu 'Yesu ana uwezo juu ya vyote'. Unaweza kuchagua kufanya hivi kwa kuwafanya watoto waigize simulizi zote kutokana na wanachokumbuka. Pia warudie mistari yote ya kukumbuka.

## Mafundisho ya Yesu

### 13. Mfano wa mpanzi – Marko 4:1-20

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Mfano huu wa Yesu unaonyesha jinsi watu wanavyoliitikia Neno la Mungu kwa namna mbalimbali. Wengine walipuuza, wengine walipenda mwanzoni lakini waliacha wanapopita kwenye magumu na wengine walisikia na kulitii na maisha yao hubadilika.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Tunahitaji kujiuliza kuwa mioyo yetu ni ya namna gani. Je, moyo wako unafanana na njia, au kwenye miamba, au kwenye miiba au udongo ulio mzuri?
- Kukaa na Mungu tukisoma Biblia na kuomba, kutatusaidia kuwa na moyo unaofanana na udongo ulio mzuri.

***Mstari wa kukumbuka:*** 'Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote.' (Marko 12:30)

## 14. Mtu aliyekuwa tajiri – Marko 10:17-31

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Mtu huyu alisikitika kwa sababu alipenda mali yake zaidi kuliko Mungu, na hivyo ingalikuwa vigumu sana kuwagawia maskini fedha zake.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Si dhambi kuwa na mali, lakini Mungu anaomba tumweke yeye kipaumbele na kumpenda zaidi kuliko mali zetu zote.
- Unawezaje kushirikiana na wengine katika vyote ulivyo navyo? Mwombe Mungu akusaidie kuwa mtu mkarimu badala ya mwenye tamaa.

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 12:30

## 15. Swali juu ya kulipa kodi – Marko 12:13-17

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu ni mwenye busara.
- Yesu anatuambia kwamba tuitolee serikali vilivyo vyao (kodi), na tumtolee Mungu vilivyo vyake (sisi wenyewe – maisha yetu).

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Tunawezaje kujitoa kwa Mungu? Kwa kutoa muda wetu na vitu vyetu kwa ajili ya mapenzi ya Mungu (kwa mfano, kwa kuwaambia marafiki zetu kuhusu Yesu, kwa kusoma Biblia n.k.)

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 12:30 *(Au 2 Wakorintho 9:7c Mungu anapenda mtu anayetoa kwa moyo.)*

## 16. Amri kuu – Marko 12:28-34

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Biblia inatufundisha kwamba cha kwanza katika maisha yetu kiwe kumpenda Mungu na kuwapenda jirani zetu.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Unawezaje kuonyesha upendo wa kweli kwa wengine, hata wale ambao si marafiki zako?

***Mstari wa kukumbuka:*** "'Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote.' Na sheria ya pili kwa ukuu ndio hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.' Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi." (Marko 12:30-31)



## 17. Sadaka ya mama mjane – Marko 12:41-44

***Kweli kuu za kufundisha (Vipengele vikuu vya simulizi)***

- Yesu alimsifu mama mjane aliyeweza kutoa kiasi kidogo sana kwa Mungu, kwa kuwa alitoa yote aliyokuwa nayo.

***Jinsi somo linavyoweza kutumika***

- Moyo wa utoaji ni muhimu kuliko kiasi tunachotoa – Mungu anafurahi tunapotoa fedha zetu na muda wetu kwa moyo wa furaha. Tusitoe fedha ili tuonekane mbele ya wengine!

***Mstari wa kukumbuka:*** Rudia Marko 12:30-31 *(Au rudia 2 Wakorintho 9:7c)*

## 18. Somo la marudio

Kabla ya kuanza dhamira inayofuata, urudie masomo yote yanayohusu 'Mafundisho ya Yesu'. Unaweza kuchagua kufanya hivi kwa kurudia kwa pamoja mstari wa kukumbuka (Marko 12:30-31) na kisha kuwauliza watoto maswali mawili yafuatayo. Katika kujibu maswali, watoto wazingatie yote waliyojifunza katika masomo matano yaliyopita.

1. Tunawezaje kuonyesha kwamba tunampenda Mungu kwa moyo wetu wote? (Majibu: Kwa kukaa na Mungu tukisoma Biblia na kuomba, kwa kumweka Mungu kipaumbele na kumpenda zaidi kuliko mali zetu zote, kwa kutoa muda wetu na vitu vyetu kwa ajili ya mapenzi ya Mungu).
2. Tunawezaje kuonyesha kwamba tunawapenda majirani zetu? (Majibu: Kwa kushirikiana na wengine katika vyote tulivyo navyo, kuwaambia kuhusu Yesu n.k.)

Andika mstari wa kukumbuka kwenye vipande vikubwa vya karatasi. Watoto wavipambe. Mwishoni, vibandikwe kwenye kuta za darasa.